EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

# MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI HUDUMA ZA UTEKELEZAJI WA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI KWA WAGUSWA WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) – KUMBUKUMBU NA. 0010006713

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalika makampuni yenye uzoefu na sifa kuonyesha nia ya kutoa huduma za utekelezaji wa uhamishaji watu na makazi katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalopita nchi mbili kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania ili kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia eneo la Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka eneo la Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Bomba lina urefu wa kilomita 1,443, ambapo kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania, bomba litakatiza Mikoa nane (8), ambayo ni; Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Bomba litapita katika Mamlaka za Halmashauri za Wilaya 27 na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mradi unahitaji mkuza kwa ajili ya bomba na miundo mbinu husika ya juu ya ardhi na kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa bomba la Mafuta ghafi. Utwaaji wa ardhi utasababisha uhamishaji wa Waguswa kutoka katika maeneo yao na shughuli zao za kiuchumi katika mkuza wa bomba, kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa katika Mipango ya Uhamishaji Watu na Makazi iliyoidhinishwa.

Kampuni inahitaji kampuni za Kitanzania zinazotoa huduma za ushauri wa maswala ya kijamii zenye sifa, uzoefu na zinazoweza kutoa huduma za utekelezaji wa Uhamishaji wa Watu na Makazi kwa Waguswa wa Mradi.

Mawanda ya kazi ni pamoja na:

- Kupanga mchakato wa uhamishaji na kuandaa Waguswa wa Mradi kwa ajili ya kuhamishwa kutoka maeneo yao na shughuli za kiuchumi kwa kushirikiana na timu ya EACOP;
- Kubainisha mahitaji na kutoa usaidizi unaohitajika kwa Waguswa wa Mradi walio katika hali hatarishi pamoja na kaya zao ambazo zimehamishwa kimakazi au kiuchumi;
- Kuwasaidia Waguswa wa Mradi wakati wa kufahamishwa stahiki zao, kusaini mikataba ya fidia na mchakato wa malipo ya fidia haswa Waguswa wa Mradi walio katika hali hatarishi;
- Kuwezesha Waguswa wa Mradi wenye makaburi kuhusiana na uhamishaji wake, ikiwemo kuwasaidia kupata vyeti vya vifo, kupata maeneo mbadala ya maziko na kuwezesha taratibu zinazohitajika za kimila/kiutamaduni ya kurudia maziko;
- Kuwezesha Waguswa wa Mradi kuhamia katika nyumba mbadala pamoja na kaya za na mali zao (ikiwemo Wanyama) na kufuatilia maendeleo yao kwa kipindi cha miezi 6;
- Kufuatilia uhamishaji wa Waguswa wa Mradi waliohamishwa kiuchumi katika ardhi mbadala;
- Kufuatilia usalama wa chakula kwa Waguswa wa Mradi wanaopokea usaidizi wa kipindi cha mpito; na
- Utoaji wa mafunzo ya usimamizi wa fedha na mipango ya fedha katika kaya kwa Waguswa wa Mradi.

Mawanda haya yamegawanywa katika vipengele vya mikoa (moja kila mkoa – vipengele 8 kwa ujumla). Mikoa ina idadi ya Waguswa wa Mradi kama ifuatavyo: Kagera 2094, Geita 1419, Shinyanga 615, Tabora 924, Singida 1231, Dodoma 808, Manyara 474, na Tanga 1557.

KAMPUNI itaruhusu Wa/Mkandarasi kuwasilisha mapendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja au Zaidi.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa watendaji wakuu katika vyombo vya kitaaluma au mashirika.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Idhini ya Malipo ya Kodi Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Maelezo mafupi ya uzoefu wa kutoa huduma za ushauri za maswala ya kijamii pamoja na utekelezaji wa shughuli za uhamishaji wa watu na makazi chini ya sheria za Tanzania na viwango vya Kimataifa vya Uwezeshaji wa Kifedha (IFS) kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania na katika jamii za vijijini.
- Wataalamu wanaopendekezwa kufanya kazi hii, ikiwemo wataalamu wa masuala ya kijamii pamoja na uzoefu wao katika kutoa huduma hizo.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA
(LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha majibu ya nia kwa ombi hili
yanahimizwa..

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza (Tafsiri hii haipo kwenye sentensi ya Kiingereza hapo juu) pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **mihye.allaire@external.total.com** na nakala kwa talal.mufti@external.total.com (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni Majira** ya Afrika Masharíki, tarehe **30th April 2021**.

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya taarifa ya kuonyesha nia yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.**